



**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 15 Septemba, 2023**

**Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.**

**I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

13. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna baadhi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGO's) zinafanyakazi hapa Zanzibar kwa kufuata vyema sheria na taratibu zilizowekwa, lakini pia zipo baadhi yao hazizishirikishi taasisi za Serikali ambazo zinatakiwa zifanye kazi nazo katika masuala mbali mbali.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi inapotokea jambo kama hili.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

41. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ni kwa kiasi gani tafiti mbali mbali za wahitimu wa vyuo vikuu vyetu zimekuwa zikitumika Serikalini kama ni sehemu ya utatuzi na suluhisho kwa miradi mbali mbali ya kimaendeleo.

### Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

30. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Inasemekana kuwa baadhi ya mimea huathiriwa na wadudu waharibifu katika hatua za uzalishaji. Wadudu hawa ni wavamizi kutoka mataifa ya nje.

Je, ni upi mkakati wa Wizara wa kuwatokomeza wadudu aina ya nzi waharibifu ili wasiendelee kudumaza, kuyaharibu pamoja na kupunguza uzalishaji wa mazao yetu mbali mbali.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

22. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mabaraza ya watoto na vijana kwa ngazi ya shehia, yanaonekana kudorora na kupungua kasi kiutendaji. Mabaraza hayo hapo mwanzoni yalifanya vizuri sana hasa kwa kufanya mikutano yao vizuri, tofauti na hali ilivyo hivi sasa.

- (a) Je, kuna mapungufu gani yaliyoyapelekea Mabaraza hayo kupoteza mwelekeo.
- (b) Je, kuna sababu gani zinazopelekea hivi sasa watoto na vijana kutokuwa na nidhamu hata kwa wazee wao seuze wazee wa wenzao.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

95. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni tu makampuni ya simu kwa ushirikiano mkubwa na TCRA yalifanya zoezi la usajili na uhakiki wa namba za simu kwa wateja wote kwa lengo la kutambuliwa wateja hao pale itakapohitajika ili kupunguza matumizi mabaya ya namba za simu. Kwa vile zoezi hili limemalizika na agizo limetolewa la kuzifungia namba zote ambazo hazijasajiliwa.

- (a) Je, ni kwa nini wimbi la meseji za simu (sms) za utapeli limeongezeka bila ya kuchukuliwa hatua stahiki.
- (b) Je, kupitia zoezi hili na hali inayoendelea hadi sasa, ni wahalifu wangapi wa simu wametiwa hatiani kwa makosa haya.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

23. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Zaidi ya mara tatu tumekuwa tukiliripoti tatizo la kuwepo umeme hafifu maeneo ya Meli Nne bila ya kupatikana ufumbuzi wowote.

Je, Wizara yako haioni kwamba kwa sasa ni muda muafaka wa kuliondoshwa tatizo hili ili kupisha shughuli za wananchi za kiuchumi na kijamii ziendelee.

III. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,  
15 Septemba, 2023.

  
(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA.**